Toleo la 26

# jarida la WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Jarida la Mtandaoni | www.michezo.go.tz | Julai 02, 2022



# Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo

# TAHARIRI

## HONGERA WIZARA KWA KUTEKELEZA AGIZO LA RAIS



Mhariri
**JOHN MAPEPELE**

Wakati makabila yote ya Tanzania yamejumuika pamoja kwenye Tamasha la kihistoria la kwanza la kitaifa la Utamaduni linalozinduliwa leo, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo. Mhe, Mohamed Mchengerwa ameteua na kuitangaza Kamati maalum ya Wadau wa Hakimiliki ambayo itajadili na kupendekeza namna bora zaidi ya kusimamia Hakimiliki nchini.

Mhe. Mchengerwa ameitangaza kamati hiyo Julai 1, 2022 akiwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam ambako Tamasha hilo la utamaduni linafanyikia na akapata fursa ya kujionea ngoma za asili za makabila mbalimbali pamoja na vyakula vya makabila tofauti.

Akitangaza uteuzi huo amesema kuwa ameamua kuteua kamati hiyo kutokana na malalamiko kutoka kwa wadau hasa wa Sekta ya Sanaa nchini kuhusiana na namna mirabaha inavyokusanywa na kugawanywa, kuwepo kwa vitendo vya uharamia katika kazi zao na elimu duni kwa wadau kuhusu masuala hayo.

Aidha, amefafanua kwamba kamati hiyo imeundwa kutokana na maelekezo aliyoyatoa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mhe, Samia Suluhu Hassan hivi karibuni ya kutaka kupatiwa ufumbumbuzi wa Hakimiliki kwa wasanii.

Tunapongeza hatua hiyo kwa kuwa inakwenda kutoa suluhisho la kudumu la kilio cha muda mrefu kwa wasanii hapa nchini. Kwa upande mwingine, tunaamini kuwa wasanii wanakwenda kufaidi jasho la kazi zao na hiyo itawafanya waweze kufanya kazi zenye ubora zaidi ambazo zitapata masoko mazuri zaidi.

Tunaungana na Kaulimbiu ya tamasha hili la Utamaduni la Kitaifa inayosema "utamaduni wetu, Fahari yetu Tujiandae kuhesabiwa, Kazi iendelee".


**BODI YA WAHARIRI**

Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo
**Dkt. Hassan Abbasi**

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo
**Saidi Yakubu**

Mhariri
**John Mapepele**

Waandishi
**Eleuteri Mangi**
**Shamimu Nyaki**
**Eliphace Marwa**

Wapiga Picha
**Joseph Kigingi**
**Projestus Binamungu**

Msanifu
**Abubakar W Kafumba**




# Tutapeleka Sanaa na Utamaduni wa Tanzania Nje ya Mipaka - Mhe. Mchengerwa

Na Shamimu Nyaki - **WUSM, Dar es Salaam**

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe.Mohamed Mchengerwa amesema Sekta ya Utamaduni na Sanaa zina mchango chanya katika kutangaza nchi ambapo ameeleza dhamira ya kuzifikisha katika mipaka ya Tanzania.

Mhe.Mchengerwa amesema hayo leo Julai 01, 2022 katika Mkutano na Wanahabari uliofanyika Uwanja wa Uhuru sehemu ambayo linafanyika Tamasha la kwanza la kihistoria la Utamaduni nchini, ambapo ameeleza namna ushiriki wake katika Tuzo za BET Awards Mwaka huu zilivyompa mawazo mapana katika kuboresha sanaa hapa nchini.

"Tutaandaa Mpango wa muda mfupi na mrefu ambao utalenga kutufikisha walipofika wenzetu, Tuzo zile zimetupa fursa ya kukutana na wadau wakubwa wa Sanaa Ulimwenguni, hivyo tutaandaa Timu ya wadau kuona hatua za kuchukua kuingia katika Tuzo zile na pia na sisi tushinde, Amesisitiza Mhe. Mchengerwa.

Ameongeza kuwa katika Sekta ya Michezo tayari ameshafanya Mazungumzo na Balozi wa Qatar hapa nchini Mhe. Hussain Ahmad kuhusu namna Tanzania itakavyoshiriki kwenye Kombe la Dunia ikiwemo kujifunza namna Bora ya kuandaa mashindano ya Kimataifa, kutokana na Nia ya kuandaa AFCON mwaka 2027.

Aidha, Mhe. Mchengerwa ameeleza kuwa wizard imefanya mageuzi Makubwa katika Mifumo ya Taasisi zake za COSOTA, Bodi ya Filamu na BASATA ili kuona namna bora ya kukusanya Mirabaha na kuweka mazingira wezeshi yatakayofanya Wasanii kufaidika na kazi zao.

Hata hivyo, ameteua Kamati itakayoshughulikia mfumo wa Hakimiliki ili Wasanii wanufaike na kazi zao.



# Naibu Waziri Gekul: Tumejipanga Kuendeleza Mashindano ya Utamaduni Kila Mwaka

Na Eleuteri Mangi - **WUSM, Dar es Salaam**

Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Pauline Gekul amefungua mashindano ya Utamaduni yanayohusisha ngoma na vyakula vya asili kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar na kuhimiza mashindano hayo kufanyika kila mwaka.

Mashindano hayo yamefunguliwa Julai 1, 2022 jijini Dar es Salaam katika Uwanja wa Uhuru ambapo Mhe. Gekul amewaeleza wananchi kuwa wizara hiyo haina jambo dogo, hivyo wamejipanga vyema kuendeleza mashindano ili yafayike kila mwaka kwa mzunguko mikoa yote.

"Leo ni siku ya kipekee, hili ni tukio la kihistoria, ni mara ya kwanza tamasha hili la kitaifa kuandaliwa, tamasha la mwaka huu ni mwanzo wa kufanyika kwa matamasha haya nchi nzima kwa kuzunguka mikoa yote, muioneshe dunia kuwa Tanzania ni tajiri wa Utamaduni na umahiri wake" amesema Mhe. Gekul.

Aidha, amesisistiza kuwa kumalizika kwa tamasha la mwaka huu, ni mwanzo wa maandalizi ya tamasha la mwaka 2023 na mikoa itajulishwa mapema ili mashindano hayo yaanzie ngazi ya kata, wilaya, mkoa na hatimaye yafanike kitaifa.

Akimkaribisha Mgeni rasmi kufungua mashindano hayo, Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo Bw. Saidi Yakubu amesema Tamasha la Kwanza la Utamaduni la Kitaifa ambalo linaendelea katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es salaam, Julai 2, 2022 litaanza na matembezi ya kiutamaduni katika jiji la Dar es salaam ambayo yatapokelewa na Mhe. Kassim Malaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia atazindua rasmi tamasha hilo.



# Mhe. Pauline Gekul ahimiza kuonesha Dunia Utamaduni wa Mtanzania

Na Shamimu Nyaki - **WUSM, Dar es Salaam**

Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Pauline Gekul, amewasili Uwanja wa Uhuru Dar es Salaam Julai 01, 2022 ambapo Tamasha la Kwanza Kitaifa la Utamaduni limeanza katika Uwanja wa Uhuru Dar es Salaam.

Mhe.Gekul, ameambatana na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Saidi Yakubu, na Viongozi wengine amewahimiza washiriki wa mashindano hayo kuyatumia kama njia ya kuonesha dunia utamaduni wetu ambapo Tamasha la Kwanza Kitaifa la Utamaduni limeanza Julai 1 hadi 03, 2022.

Mabanda ya Mikoa mbalimbali yamesheheni vitu mbalimbali vya asili vya kiutamaduni ambao ni tunu kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.




# Chifu Kingalu Apongeza Serikali Kujali na Kulinda Utamaduni wa Mtanzania

Na Eleuteri Mangi – **WUSM, Dar es Salaam**

Serikali inaendelea kufanya kazi vizuri ambapo Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo inaendelea kushirikiana na kufanya kazi na makabila yote nchini ili kuendeleza mila njema kwa vizazi vijavyo.

Hayo yamesemwa na Chifu Kingalu XV Mwanabanzi II wa Morogoro Hussein Ally Machaga Julai 1, 2022 mara baada kufunguliwa kwa mashindano ya ngoma na vyakula vya asili na Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Pauline Gekul ambayo yanaendelea katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam wakati wa Tamasha la Kwanza la Utamaduni Kitaifa.

"Machifu tunaenziwa sana, Rais Samia Suluhu Hassan anachokifanya anafuata nyayo za watangulizi wake anaamsha ari ya Machifu kusimamia mila na desturi njema kwa watoto wetu" amesema Chifu Kingalu.

Chifu huyo amesisistiza Utamaduni ni hazina ambayo kila kabila na taifa wanapaswa kuulinda na kuendeleza kwa kizazi hadi vizazi vijavyo na kusisitiza tamasha hilo liendelezwe na kudumishwa ili lisipotee.

Aidha, Chifu Kingalu amesisitiza kuwa kila mtu kwenye eneo lake atumie mazingira yake vizuri kwa kupanda miti ya asili ikiwemo ya matunda ili kuimarisha afya zao kwa kula vyakula vya asili.

Ameuongeza kuwa ipo miti pesa ambayo inamanufaa kiuchumi ikiwemo mikarafuu ambayo inakua na kuanza kuvunwa baada ya mika mitano na kudumu hadi miaka 100 pamoja na amdalasini ambayo hupandwa na kuanza kuvuna baada ya miaka mitatu hatua ambayo itapata pesa zaidi ya kiasi anachopata sasa ili kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.










UTAMADUNI WETU
FAHARI YETU















**JAMHURI YA UUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**

**Simu:** +255 26 2322129
**Nukushi:** 255 26 2322128
**Tovuti**: www.michezo.go.tz

Mji wa Serikali,
Mtumba, Dodoma,
2 Mtaa wa Michezo,
S. L. P 25,
**40481 DODOMA.**

## TAARIFA KWA UMMA

## KAMATI YA KURATIBU NAMNA BORA YA KUSIMAMIA HAKIMILIKI NCHINI

**Julai 1, 2022 – Dar es Salaam**
Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Mohamed Mchengerwa ameteua Kamati ya Wadau wa Hakimiliki nchini ambayo itajadili na kupendekeza namna bora zaidi ya kusimamia Hakimiliki nchini;

Uteuzi huo, ni kutokana na malalamiko kutoka kwa wadau hasa wa Sekta ya Sanaa nchini kuhusiana na namna mirabaha inavyokusanywa na kugawanywa, kuwepo kwa vitendo vya uharamia katika kazi zao na elimu duni kwa wadau kuhusu masuala hayo.

Majina ya Wajumbe wa Kamati hiyo ni:

(i) Bw. Victor Michael Tesha – (Mtaalam wa Fedha na Masoko) - **Mwenyekiti**
(ii) Dkt. Saudin Mwakaje – Mtaalam wa Hakimiliki – Chuo Kikuu cha Dar es Salaam- **Makamu Mwenyekiti**
(iii) Bw. Dimesh S. Mawj – Mtaalamu wa Sheria ya Maliakili (Intellectual Property Law) - **Katibu**

**Wajumbe**
(i) Mhe. Hamis Mwinjuma – (Mwana FA) Mbunge na Msanii Mkongwe -
(ii) Dkt. Omary Mohamed - Kamishna wa Utamaduni Zanzibar
(iii) Bw. Paul Mattysse (P Funk) - Mzalishaji wa Muziki
(iv) Bi. Safina Kimbokota – Msanii wa Sanaa na Ufundi
(v) Bw. Torriano Saramba – Mdau wa Hakimili Mtandaoni
(vi) Bw. Gabriel Kitua – Mwenyekiti Chama cha Wachapishaji
(vii) Bw. Twiza Mbarouk – Shirikisho la Filamu
(viii) Dkt. Asha Salum Mshana – Mkurugenzi Msaidizi Haki za Wasanii.

Kamati itaanza kutekeleza majukumu yake Julai 01, 2022

John Mapepele
**MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

# WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano
Serikalini - GCU

**Mawasiliano**

P.O. Box 25, Dodoma,Tanzania
Mji wa Serikali Mtumba
Telephone: +255 26 2322 129
Nukushi: +255 26 2322 128
Barua pepe: km@habari.go.tz